swahili

# L'Éternel regarde au cœur

Par Ronald M. Barcellos
*des soixante-dix*

# Bwana Hutazama Moyo

Mzee Ronald M. Barcellos
*Wa Sabini*

Conférence générale d'octobre 2025

---

*Il nous suffit de tourner pleinement notre cœur vers Dieu pour qu'il accomplisse ses desseins et nous transforme en ce qu'il veut que nous soyons.*

*Simulizi hii hutufundisha kwamba yote ambayo Mungu anahitaji kukamilisha kusudi lake na kutusaidia kuwa tunavyopaswa kuwa ni kwa kila mmoja wetu kugeuza kikamilifu mioyo yetu kumulekea Yeye.*

Lorsqu'il a reçu le commandement de choisir le nouveau roi d'Israël parmi les fils d'Isaï, le prophète Samuel, en voyant Éliab, le fils aîné d'Isaï, s'est exclamé : « Certainement, l'oint de l'Éternel est ici devant lui. » Mais Éliab n'était pas le serviteur choisi de l'Éternel. Le Seigneur a averti Samuel : « Ne prends point garde à son apparence et à la hauteur de sa taille, car je l'ai rejeté. L'Éternel ne considère pas ce que l'homme considère ; l'homme regarde à ce qui frappe les yeux, mais l'Éternel regarde au cœur. »

Même si David n'était pas physiquement le plus fort ou le plus habile de ses frères, son cœur était grand aux yeux de Dieu. David aimait Dieu de tout son cœur et avait le profond désir de lui obéir. Il avait une foi inébranlable en l'amour de Dieu, en son pouvoir et en ses bénédictions promises, comme il l'a démontré plus tard, en triomphant courageusement de Goliath, avec l'aide du Seigneur.

Cette histoire nous enseigne qu'il nous suffit de tourner pleinement notre cœur vers Dieu pour qu'il accomplisse ses desseins et nous transforme en ce qu'il veut que nous soyons. À un docteur de la loi, il a commandé : « Tu aimeras le Seigneur, ton Dieu, de tout ton cœur. » À Joseph Smith, le prophète, il a dit : « Voici, le Seigneur exige le cœur, et un esprit bien disposé. » Et aux Néphites, le Sauveur ressuscité a lancé cette invitation : « Vous m'offrirez en sacrifice un cœur

wakati alipoamriwa kumchagua mfalme mpya wa Israeli kati ya wana wa Yese, nabii Samweli, baada ya kuwa amemwangalia Eliabu, mwana mkubwa wa Yese, alistaajabu kwa ari, "Yakini masihi wa BWANA yupo hapa mbele zake." Lakini Eliabu hakuwa mtumishi aliyeteuliwa wa Bwana. Mwokozi alimwambia Samweli: "Usimtazame uso wake, wala urefu wa kimo chake; kwa maana mimi nimemkataa: Bwana haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo."

Wakati Daudi akiwa si mwenye umbo la mtu mwenye nguvu sana au mwenye ujuzi zaidi ya kaka zake, moyo wake ulikuwa imara mbele za Mungu. Alimpenda Mungu kwa moyo wake wote na alikuwa na hamu kubwa sana ya kumtii. Alikuwa na imani isiyotikisika kwenye upendo wa Mungu, nguvu na baraka zilizoahidiwa kama baadae alivyodhihirisha wakati kwa ujasiri alipopambana na kumshinda Goliati kwa msaada wa Bwana.

Simulizi hii hutufundisha kwamba yote ambayo Mungu anahitaji kukamilisha kusudi lake na kutusaidia kuwa tunavyopaswa kuwa ni kwa kila mmoja wetu kugeuza kikamilifu mioyo yetu kumulekea Yeye. Kwa mwana sheria, Aliamuru, "Nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote."Kwa Nabii Joseph Smith, Alisema, "Tazama, Bwana anahitaji moyo na akili yenye kukubali."Na kwa Wanefi, Mwokozi aliyefufuka alitoa mwaliko huu: "Na mtatoa kwangu dhabihu

brisé et un esprit contrit. »

Pourquoi en est-il ainsi ? Le Sauveur a enseigné que, grâce à son sacrifice expiatoire, si notre cœur est entièrement tourné vers lui, nous recevrons la force et les dons spirituels nécessaires pour surmonter les difficultés de la condition mortelle, résister à la tentation, être guidés, acquérir de l'intelligence, et ressentir la joie et la paix dans notre vie. « C'est des petites choses que sort ce qui est grand. » Le Seigneur a dit qu'il peut rendre « fortes les choses qui sont faibles», et nous donner tout ce dont nous avons besoin pour réussir dans cette vie et recevoir la vie éternelle. Il a déclaré : « Heureux ceux qui ont le cœur pur, car ils verront Dieu! »

Je crois que c'est la raison, au moins en partie, pour laquelle Jésus-Christ a si souvent corrigé les scribes et les pharisiens pendant son ministère dans la condition mortelle. Bien que diligents à respecter sa loi, ils le faisaient pour de mauvaises raisons. Il les a réprimandés, disant : « Ce peuple m'honore des lèvres, mais son cœur est éloigné de moi. »

C'est un rappel sérieux à tous ses disciples qu'il ne s'agit pas seulement de nos paroles et nos actions, mais aussi de la raison pour laquelle nous obéissons à Jésus-Christ, c'est-à-dire nos désirs et nos motivations. Il a dit : « Car moi, le Seigneur, je jugerai tous les hommes selon leurs œuvres, selon le désir de leur cœur. » Notre Père céleste veut plus que des actes machinaux d'obéissance et de service de la part de ses enfants. Il veut que nous fassions ces choses avec une intention réelle, parce que nous l'aimons de tout notre cœur. Il veut que nous devenions semblables à lui.

Si la santé spirituelle de notre cœur est une préoccupation essentielle du Sauveur, ce qu'il recherche chez un véritable disciple, comment pouvons-nous examiner notre cœur et savoir s'il est juste aux yeux de Dieu ?

Récemment, alors que ma femme et moi rentrions de notre mission au Portugal, nous avons fait une série d'examens de santé pour évaluer notre condition physique. Certains de ces examens portaient sur la santé de notre cœur : des analyses de sang, un échocardiogramme et un test de résistance à l'effort. Le Sauveur nous a également donné une série d'examens spirituels grâce auxquels nous pouvons évaluer l'état spirituel de notre cœur. En voici quelques-uns :

ya moyo uliopondeka na roho iliyovunjika."

Je, kwa nini hivyo? Mwokozi alifundisha kwamba ikiwa mioyo yetu itamgeukia yeye kikamilifu, kwa sababu ya dhabihu Yake ya kulipia dhambi, tunaweza kubarikiwa kwa nguvu na vipawa vya kiroho ambavyo tunahitaji ili kushinda changamoto za maisha yetu duniani, kukinzana na majaribu na kupokea mwongozo na uelewa, na kuhisi shangwe na amani maishani mwetu. Na kutokana na mambo madogo huja yale yaliyo makuu."Alisema Yeye anaweza "kuvifanya vitu vidhaifu kuwa vyenye nguvu"na kutubariki kwa kila kitu tunachohitaji ili kufanikiwa katika maisha haya na kupokea uzima wa milele. "Wamebarikiwa wasafi wa moyo, " Alisema "kwani watamwona Mungu."

Ninaamini hii ndio sababu, angalau kwa sehemu fulani, Yesu Kristo mara kadhaa aliwasahihisha waandishi na Mafarisayo wakati wa huduma yake duniani. Ingawa walikuwa mahiri kwenye kushika sheria Zake, walifanya hivyo kwa sababu zisizo za kweli.Aliwaonya, akisema, "Watu hawa huniheshimu kwa midomo; Ila mioyo yao iko mbali nami."

Huu ni ukumbusho wa muhimu kwa wafuasi Wake wote kuwa si kuhusu tunayofanya pekee—maneno na matendo yetu— lakini pia kuhusu kwa nini tunafanya ambacho Yesu Kristo ametuamuru kufanya—tamanio na nia zetu. Alisema, "Kwani Mimi, Bwana, nitawahukumu watu wote kulingana na matendo yao, kulingana na tamaa za mioyo yao."Baba yetu wa Mbinguni anatamani zaidi ya matendo ya kukaririwa ya utiifu na huduma kutoka kwa watoto Wake. Anatutaka tufanye vitu vyema kwa nia ya dhati, kwa sababu tunampend Yeye kwa mioyo yetu yote. Anatutaka tutamani kuwa kama Yeye.

Sasa, ikiwa afya yetu ya kiroho ni kitu ambacho Mwokozi anajali—anachokitazama kwa mfuasi wa kweli—basi tunawezaje kuichunguza mioyo yetu na kujua ikiwa iko sahihi mbele za Mungu?

Hivi karibuni, wakati mke wangu pamoja nami tuliporudi kutoka kwenye misioni yetu huko Ureno, tulifanya vipimo vya afya kutathimini hali zetu. Baadhi ya vipimo hivyo vilifokasi kwenye afya ya moyo—kama vile vipimo vya damu, vipimo vya kuonyesha ndani ya moyo na uwezo wa moyo wa usukumaji damu. Ninaamini kwamba Mwokozi pia ametupatia seti ya vipimo vya kiroho ili kutathimini hali za kiroho za mioyo yetu. Acha nishiriki nanyi baadhi ya

hivyo.

## Évaluer son cœur à l'aide de tests spirituels

« Car là où est ton trésor, là aussi sera ton cœur», a enseigné Jésus. Un trésor est quelque chose de précieux pour nous, une chose à laquelle nous consacrons des efforts et de l'attention. Notre manière d'occuper notre temps, l'objet de notre attention et les raisons qui nous poussent à agir en disent long sur notre cœur. Le Sauveur nous a avertis que, bien qu'il en appelle beaucoup, peu sont élus « parce que leur cœur se porte tellement vers les choses de ce monde et [qu'ils] aspire[nt] tant aux honneurs des hommes». Est-ce que je fais du Sauveur une priorité dans ma vie ? Mon œil est-il fixé uniquement sur sa gloire dans tout ce que je fais ?

Tout au long des Écritures, le Seigneur et ses prophètes associent l'orgueil et la désobéissance à l'endurcissement de cœur. Néphi a exhorté ses frères en disant : « Comment se fait-il que vous ne gardiez pas les commandements du Seigneur ? Comment se fait-il que vous vouliez périr à cause de l'endurcissement de votre cœur? » Le Seigneur a mis en garde les saints au Missouri en leur disant : « Mais celui qui ne fait rien tant qu'on ne le lui a pas commandé et qui reçoit un commandement le cœur indécis et le garde avec paresse, celui-là est damné. » Même si le Sauveur n'attend pas la perfection dans l'obéissance à ses commandements, il nous demande d'avoir le désir sincère de les respecter et de nous efforcer de le faire de tout notre cœur.

Le Seigneur a lancé l'exhortation suivante à Oliver Cowdery : « Conserve précieusement ces paroles en ton cœur. » Nous sommes invités à sonder diligemment les Écritures et, par le pouvoir du Saint-Esprit, à obtenir la compréhension et le témoignage de la véracité de l'Évangile dans notre cœur.

Le prophète Abinadi a réprimandé les prêtres du méchant roi Noé pour ne pas avoir fait cela, disant : « Vous n'avez pas appliqué votre cœur pour avoir l'intelligence ; c'est pourquoi vous n'avez pas été sages. » Est-ce que je fais un effort sincère pour étudier quotidiennement les Écritures et appliquer mon cœur pour les comprendre par la prière ?

Le Sauveur a enseigné que « c'est du cœur que viennent les mauvaises pensées» et que « c'est de l'abondance du cœur que la bouche parle». La

## Tathimini Moyo Wako kwa Vipimo vya Kiroho

"Kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwa na moyo wako,"Yesu alifundisha. Hazina ni kitu fulani chenye thamani kwetu, kitu fulani ambacho tunaweka uwezo na umakini. Sehemu tunayochagua kutumia muda na umakini wetu, pia kile ambacho hutuhamasisha kufanya tunayofanya, huzungumza zaidi kuhusu mioyo yetu. Mwokozi alionya kwamba wengi Amewaita, lakini wateule ni wachache. "Kwa sababu mioyo yao imekuwa juu ya mambo ya ulimwengu huu, na [wanatafuta] kupata heshima kutoka kwa wanadamu."Je, ninamuweka Mwokozi kipaumbele kwenye maisha yangu? Je, jicho langu liko kwenye utukufu Wake kwenye vyote nifanyavyo?

Kote kwenye maandiko, Bwana na manabii Wake wamehusisha majivuno na kutotii ikiwa ni pamoja na kushupaza moyo. Nefi aliwasihi kaka zake, akisema: "Kwa nini hamtii amri za Bwana? Kwa nini muangamie, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu?"Kwa waumini huko Missouri, Bwana aliwaonya "Lakini yule asiyefanya lolote mpaka ameamriwa, na kupokea amri kwa moyo wenye mashaka, na kuzishika kwa uvivu, huyo amelaaniwa."Wakati Mwokozi hategemei ukamilifu katika kutii amri Zake, Yeye hatuamuru tutamani na kujitahidi kuzishika kwa mioyo yetu yote.

Bwana alimsisitiza Olive Cowdery "kuyatunza maneno haya katika moyo wako"Tunaalikwa kupekua maandiko kwa bidii na, kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu, kutafuta kuelewa na ushahidi wa ukweli wa injili katika mioyo yetu.

Nabii Abinadi aliwakanya makuhani waovu wa Mfalme Nuhu kwa kutofanya hili, akisema, "Hamjajitolea mioyo yenu kwa ufahamu; kwa hivyo, hamjawa wenye hekima."Je, ninafanya juhudi za dhati kujifunza maandiko kila siku na kujitolea moyo wangu kwenye uelewa kupitia sala?

Mwokozi alifundisha kwamba "moyoni hutoka mawazo mabaya"na kwamba "kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake."Kiwango

qualité de nos pensées et de nos paroles est un bon indicateur de la pureté de notre cœur. Ai-je trop de pensées négatives sur les actions ou les motivations d'autrui, ou sur moi-même ? Suis-je trop prompt à juger et à condamner autrui ? Est-ce que je cherche des excuses ou des justifications à mes erreurs ? Et qu'en est-il de mes paroles ? Est-ce qu'elles édifient et inspirent les personnes qui m'entourent ? Ou engendrent-elles souvent des querelles et du ressentiment?

Une fois mes examens médicaux terminés, mon médecin m'a dit que, dans l'ensemble, mon cœur était en bonne santé, mais qu'il fallait régler de petits problèmes dès maintenant, avant qu'ils ne s'aggravent. Il m'a ensuite prescrit des changements dans mon mode de vie. De même, lorsque vous effectuerez cette évaluation spirituelle de votre cœur et remarquerez la présence de certains symptômes négatifs, ne paniquez pas ! Le Sauveur a fourni d'excellents médicaments et traitements spirituels pour vous aider. Il a même promis de vous donner un cœur nouveau! Voici quelques actions qui peuvent augmenter la robustesse spirituelle de votre cœur.

## Améliorer la santé spirituelle de son cœur

Quand nous consacrons du temps chaque jour à nous rapprocher du Christ, notre cœur change. L'étude quotidienne des Écritures, accompagnée de prières sincères et de jeûnes réguliers, fera grandir votre amour pour le Sauveur, et fortifiera votre foi et votre désir de vous repentir et de livrer humblement votre cœur à Dieu. Réfléchissez à cet exemple donné par Néphi : « C'est pourquoi je criai au Seigneur ; et voici, il me visita et adoucit mon cœur, de sorte que je crus toutes les paroles qui avaient été dites par mon père. »

Si nous continuons de nourrir la semence de la foi par nos désirs et nos actions justes, nous connaîtrons la même sanctification de cœur que celle des Néphites : « Ils jeûnaient et priaient souvent, et devenaient de plus en plus forts dans leur humilité, et de plus en plus fermes dans la foi au Christ, au point que cela leur remplissait l'âme de joie et de consolation, oui, au point que cela leur purifiait et leur sanctifiait le cœur, sanctification qui venait de ce qu'ils avaient livré leur cœur à Dieu. »

Il a enseigné : « Si vous m'aimez, gardez mes commandements. » Il nous invite à montrer

cha usafi wa mawazo na maneno yetu ni kiashiria cha usafi wa mioyo yetu. Je, ninafurahia mawazo hasi kuhusu matendo au nia za wengine, au hata kuhusu mimi mwenyewe? Je, ninatoa hukumu ya haraka na kulaani wengine? Je, ninatafuta sababu au njia za kuhalalisha makosa yangu? Na vipi kuhusu maneno yangu? Je, yanawainua na kuwapa msukumo wale wanaonizinguka? Au mara zote yanatengeneza mgogoro na msuguano?

Baada ya uchunguzi wa afya yangu kukamilika, daktari wangu aliniambia kwamba, kiujumla, moyo wangu ulikuwa sawa—lakini kulikuwa na vitu vichache ambavyo vilihitajika kushughulikiwa sasa, kabla havijaleta madhara makubwa. Kisha alifafanua baadhi ya mabadiliko kwenye mfumo wa maisha. Vivyo hivyo, wakati unapofanya tathimini hii ya kiroho ya moyo wako na kugundua baadhi ya dalili hasi zikianza kunyemelea, tafadahali usihamaki! Mwokozi ametoa dawa bora zaidi ya kiroho na matibabu ili kukusaidia. Hata ameahidi kukupa moyo mpya!Haya ni baadhi ya matendo ambayo yanaweza kuboresha nguvu ya kiroho ya moyo wako.

## Boresha Afya ya Kiroho ya Moyo Wako

Tunapotoa muda kila siku kumkaribia Kristo, mioyo yetu inabadilishwa. Kujifunza maandiko kila siku, kunakosindikizwa na sala ya dhati na kufunga mara kwa mara, kutaongeza upendo wako kwa Mwokozi na kuimarisha imani yako na hamu ya kutubu na kwa unyenyekevu kuutoa moyo wako kwa Mungu.Zingatia mfano huu kutoka kwa Nefi: "Nilimlilia Bwana, na tazama akanijia mimi, na akanigusa moyo wangu kwamba nikaamini maneno yote ambayo baba yangu alikuwa ameyazungumza."

Tunapoendelea kuikuza mbegu ya imani kupitia hamu na matendo yetu matakatifu, tutapata uzoefu sawa wa utakaswaji wa moyo kama wa Wanefi: "Walakini walifunga na kuomba kila wakati, na wakapokea nguvu kwa wingi katika unyenyekevu wao, na wakawa imara zaidi na imara katika imani kwa Kristo, hadi nafsi zao zikajazwa na shangwe na faraja, ndiyo, hata kwenye kusafishwa na utakaso wa mioyo yao, utakaso ambao huja kwa sababu ya wao kumtolea Mungu mioyo yao."

Mwokozi alifundisha, " Mkinipenda, mtazishika amri zangu."Anatualika tuonyeshe upendo

notre amour en contractant et en respectant des alliances avec lui. Si nous nous efforçons quotidiennement de respecter ses commandements, de nous repentir sincèrement de nos péchés, et de persévérer à prendre son nom sur nous et à conformer notre volonté à la sienne, nous aurons la bénédiction d'avoir la compagnie constante du Saint-Esprit.

Néphi a témoigné : « Je sais que si vous suivez le Fils d'un cœur pleinement résolu, ne commettant ni hypocrisie ni tromperie devant Dieu, mais avec une intention réelle, vous repentant de vos péchés, témoignant au Père que vous êtes disposés à prendre sur vous le nom du Christ par le baptême […], alors vous recevrez le Saint-Esprit. » Le Saint-Esprit vous guidera, et vous aidera à connaître la volonté du Seigneur et à faire de bons choix.

Le Sauveur invite tout le monde à « le servir de tout [son] cœur». Lorsque nous choisissons de faire, d'un cœur sincère et avec une intention réelle, tout ce que le Seigneur nous a demandé de faire, comme respecter les commandements, prendre la Sainte-Cène, aller au temple et servir autrui, chaque acte de service et d'adoration devient une expérience spirituelle puissante qui fortifie notre foi et notre témoignage, et remplit notre cœur de joie et d'amour pour Dieu et notre prochain.

La question du prophète Alma résonne toujours aujourd'hui : « Êtes-vous nés spirituellement de Dieu ? Votre visage est-il empreint de son image ? Avez-vous éprouvé ce grand changement dans votre cœur? »

Frères et sœurs, je vous invite à donner tout votre cœur au Sauveur aujourd'hui. Que chaque acte d'adoration et de service soit sincère et délibéré. Mettez de côté les distractions du monde et consacrez du temps de qualité au Seigneur chaque jour de votre vie. Repentez-vous et revenez à lui de tout votre cœur, et il vous pardonnera et vous entourera dans les bras de son amour. Ne recherchez pas les choses de ce monde, mais choisissez d'avoir l'œil fixé uniquement sur sa gloire et de rechercher les choses d'un monde meilleur. Il connaît vos pensées et les désirs de votre cœur et, à mesure que vous viendrez à lui, il vous bénira avec la force, la confiance, la paix et la joie dans cette vie, et avec une place dans son royaume céleste pour toute l'éternité.

Je sais que Jésus-Christ vit. Il est notre

wetu kwa kufanya na kushika maagano Naye. Tunapojitahidi kila siku kushika amri Zake, kwa dhati kutubu dhambi zetu, na kuvumilia kwenye kujichukulia juu yetu jina lake na kuweka mapenzi yetu kuwa sawa na Yake, tunaweza kubarikiwa na uwepo wa daima wa Roho Mtakatifu.

Nefi alishuhudia: "Najua kwamba kama mtamtii Mwana, kwa moyo wa lengo moja, bila unafiki na udanganyifu mbele yake Mungu, lakini kwa kusudi kamili, na kutubu dhambi zenu, mkishuhudia kwa Baba kwamba mnataka kujivika juu yenu jina la Kristo, kwa ubatizo … , ndipo mtapokea Roho Mtakatifu."Roho Mtakatifu atakuongoza na kukusaidia kujua mapenzi ya Bwana na kufanya chaguzi njema.

Mwokozi anawaalika wote "kumtumikia kwa moyo wote."Wakati tunapochagua kufanya kila kitu ambacho Bwana anatuamuru kufanya—kama vile kutii amri zake, kushiriki sakramenti, kuabudu hekaluni, na kuwatumikia wengine—kwa moyo wa dhati na kwa nia ya dhati, kila tendo la huduma na kuabudu huwa uzoefu wa kiroho wenye nguvu ambao utaimarisha imani yetu na ushuhuda na kujaza mioyo yetu kwa shangwe na upendo kwa Mungu na wenzetu.

Swali la nabii Alma bado linatoa mwangi hivi leo: "Je, mmezaliwa kiroho katika Mungu? Mmepokea mfano wake katika nyuso zenu? Mmeshuhudia mabadiliko haya makuu katika mioyo yenu?"

Akina kaka na dada, ninawaalika kuutoa moyo wako wote kwa Mwokozi hivi leo. Acheni kila tendo la kuabudu na huduma liwe la dhati na la kusudi jema. Ondoa vivuta mawazo vya ulimwengu na jitahidini kuwa na muda maalum kwa ajili ya Bwana kila siku za maisha yako. Tubu na mrudie Yeye kwa moyo wote, na Yeye atakusamehe na atakuzingira kwa mikono Yake ya upendo.Usitafute mambo ya ulimwengu huu, lakini chagua kuwa na jicho lako kwenye utukufu Wake pekee na tafuta vitu bora zaidi.Yeye anajua mawazo yako na hamu za moyo wako, na unapomwendea Yeye, Atakubariki kwa nguvu, ujasiri, amani, na shangwe katika maisha haya na sehemu kwenye ufalme Wake wa selestia milele yote.

Ninajua Yesu Kristo yu hai. Yeye ni Mkom-

Rédempteur. Et il nous aime, vous et moi, de tout son cœur. Au nom de Jésus-Christ. Amen.

bozi wetu. Na Anakupenda wewe na mimi kwa moyo wote. Katika jina la Yesu Kristo, amina.